**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA JUU YA UWASILISHWAJI WA RIPOTI YA MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU WA UCHUMI ZANZIBAR KWA KIPINDI CHA JANUARI – DISEMBA 2022

---

**Mheshimiwa Spika;** awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, Muumba wa mbingu na ardhi, Muumba uhai na uzima, kwa kutujaalia afya njema na taufiki ya kuweza kukutana hapa leo hii, kwa ajili ya muendelezo wa majukumu yetu muhimu ya kuishauri Serikali pamoja na kuwakilisha wananchi wa Zanzibar katika kufanya maamuzi muhimu ya kitaifa.

**Mheshimiwa Spika;** aidha, nitumie fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kwa ajili kutoa maoni ya Kamati yetu ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa juu ya uwasilishwaji wa Ripoti ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar kwa kipindi cha Januari – Disemaba, 2022.

**Mheshimiwa Spika;** pia, natumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa kuweza kuiwasilisha vyema mbele ya Baraza lako Tukufu, Ripoti ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar kwa kipindi kifupi cha miezi Kumi na Mbili, Ripoti hii inaakisi matokeo ya kazi nzuri zilizofanywa na Mamlaka hii katika kukamilisha majukumu yao ya msingi kama Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar, nambari 1 ya mwaka 2012, kama kifungu cha 13 cha Sheria hii kinavyoelekeza.

**Mheshimiwa Spika;** kwa namna ya pekee napenda kutoa shukrani zangu za dhati

kwa Wajumbe na Makatibu wa Kamati hii ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mashirikiano yao makubwa yanayoendelea katika Kamati hii na kutimiza wajibu wao katika chombo hiki kitukufu katika nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** naomba sasa kwa ruhusa yako kuwataja Wajumbe wanaounda Kamati hii kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Machano Othman Said - Mwenyekiti
2. Mhe. Maryam Thani Juma - Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Zaina Abdalla Salum - Mjumbe
4. Mhe. Mussa foum Mussa - Mjumbe
5. Mhe. Abdalla Abass Wadi - Mjumbe
6. Mhe: Haji Shaaban Waziri - Mjumbe
7. Mhe. Panya Ali Abdalla - Mjumbe
8. Mhe. Suleiman Haroub Suleiman - Mjumbe
9. Mhe. Mwanaisha Mohammed Kheir - Katibu
10. Ndg. Ali Alawy Ali - Katibu
11. Ndg. Shawana Mohammed Haji - Katibu
12. Ndg. Amina Abeid Hemed - Mkalimani

**Mheshimiwa Spika;** sambamba na hilo, naomba kutumia fursa hii kumpongeza kwa dhati kabisa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar Ndugu Ali Abdalla Ali kwa juhudi zake za kuleta mageuzi na mafanikio ya kazi ambayo yamepeleka kupatikana kwa Muundo wa Ofisi pamoja na Kupata Sheria Mpya ya Rushwa Namba 5 ya 2023. Aidha, Shukurani za pekee ziwaendee watendaji wote wa Mamlaka hii kwa kazi zao nzuri na ngumu wanazozifanya katika kusimamia haki na wajibu wa wananchi kwa lengo la kulinda uchumi wa Zanzibar na kuimarisha utawala bora. Hata hivyo, Mamlaka hii inakabiliwa na baadhi ya changamoto ambazo kimsingi hazirudishi nyuma juhudi zao

katika kupambania maendeleo ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika;** baada ya utangulizi huo sasa naomba kukiri kwamba Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa imeipokea na kuipitia kikamilifu Ripoti ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar, siku ya Jumatano, tarehe 06/9/2023 na kuandaa maoni na ushauri wetu juu ya ripoti hii ili kuweza kuyawasilisha mbele ya Baraza lako tukufu kwa mujibu wa taarifa zilizomo ndani ya Ripoti hii.

**Mheshimiwa Spika;** katika utekelezaji wa majukumu yake ZAECA imeeleza kwamba imepokea jumla ya malalamiko 410 yanayohusiana na mambo mbali mbali ikiwemo vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi. Kwa kuwa miongoni mwa tuhuma hizo asilimia kubwa zimekosa mashiko na kushindwa kufunguliwa Mashtaka na kupelekea kesi 18 tu kufikishwa Mahkamani kutokana na uchunguzi uliofanyika.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mantiki hiyo, Kamati haikuridhishwa na mwenendo wa uchunguzi wa mashauri hayo ambayo kwa mwaka mzima ni majalada 34 tu yaliyofanyiwa uchunguzi kupitia ZAECA. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali ili kuhakikisha Mamlaka hii inafanya kazi zake kwa ubora na kwa kuzingatia wakati mahususi basi ni lazima kuongezwa nguvu kwa kupatiwa rasilimali watu wa kusimamia masuala haya pamoja na rasilimali fedha, sambamba na kuongezwa kwa vitendea kazi ili mashauri hayo yaweze kumalizika kwa haraka.

**Mheshimiwa Spika;** kwa upande mwengine, Kamati imeshtushwa na taarifa zinazohusiana na tuhuma za matumizi mabaya ya mali za Ofisi pamoja na ubadhirifu wa mali na mapato ambapo inaonekana kushamiri kwa makosa haya katika taasisi za umma. Kwa msingi huo, Kamati inashauri kitengo cha ukaguzi wa ndani kwa kila taasisi kuhakikisha kimesimamia vyema taratibu za ukaguzi wa mali na vifaa ili kuhakikisha matumizi bora ya ofisi na mali zake. Aidha, Kamati inashauri hatua kali za kisheria kuchukuliwa kwa watendaji wenye kuonyesha tabia za matumizi mabaya ya ofisi sambamba na kutumia nafasi zao kwa kujinufaisha kimapato.

**Mheshimiwa Spika;** Katika kurahisisha huduma za mawasiliano na kuwapatia wananchi wepesi wa kutoa taarifa kwa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi, Mamlaka imeandaa namba ya simu ya bure kwa ajili ya kutolea taarifa zinazohusiana na masuala ya rushwa na uhujumu uchumi ili kuwarahisishia

wananchi kutoa taarifa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Ofisi kwa kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusiana na umuhimu wa matumizi ya namba hiyo ya bure ambayo ni 113. Hata hivyo, kamati inakemea vikali kwa baadhi ya wananchi kupiga simu kwa kufanya mzaha kwa Mamlaka jambo ambalo linasababisha uzorotaji wa kazi kwa kiasi kikubwa. Sambamba na hilo, Kamati inaelekeza kuchukuliwa hatua kali kwa yeyote anayekwenda kinyume na agizo hilo pindi atakapobainika akitenda kosa hilo.

**Mheshimiwa Spika;** kufuatia Mamlaka kuendelea na zoezi la uokozi wa fedha zinazopatikana kwa njia ya rushwa na uhujumu uchumi kwa mwaka 2022. Kamati inaipongeza Mamlaka kwa kufanikisha kuokoa kiasi cha Fedha za Kitanzania Shilingi Bilioni Tatu Milioni Mia Saba Sabini Laki Mbili Thalathini na Tano Elfu Mia Tano Arubaini na Nane nukta Tisa Tisa (3,770,235,548.99/=) na kuzirejesha Serikalini. Kwa mantiki hiyo, Kamati inaiomba Serikali kulifikiria tena suala la kuwapatia ZAECA kiasi kidogo yaani fungu dogo la fedha kutokana kiasi wanachookoa ambapo ni uthibitisho dhahiri kwenye ufanisi wa kazi zao.

**Mheshimiwa Spika;** katika sura ya tatu ya ripoti hii inayozungumzia masuala ya kinga dhidi ya rushwa, Kamati imeridhika na Mamlaka kwa kufanikiwa kutoa ushauri katika taasisi mbali mbali juu ya namna bora ya kujikinga na vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi, kufuatilia na kushauri Miradi ya Maendeleo ili kuendana na thamani halisi ya fedha.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imegundua kuwepo kwa kasoro ya kutotajwa kwa aina ya miradi ambayo imeonekana na mapungufu, hali ambayo imepelekea Kamati kukosa uelewa wa kutosha unaohusiana na miradi hiyo. Hata hivyo, Kamati inashauri katika ripoti zinazokuja kutajwa kwa miradi yote yenye mapungufu endapo uchunguzi wa kutosha utafanyika na kuhakikisha kuwa miradi hiyo ina mapungufu kwa mujibu wa mikataba yao.

**Mheshimiwa Spika;** kufuatia zoezi la utoaji wa elimu kwa umma, Mamlaka imefanikiwa kuandaa vipindi vya redio na TV, kufanya semina na mikutano yenye kuhusisha washirika mbali mbali, kushiriki katika maadhimisho ya Siku ya Rushwa pamoja na kuandaa machapisho; Kamati inatoa pongezi kwa Mamlaka kwa

kufanikisha majukumu yake ya uelimishaji kwa umma ili kudhibiti matendo ya rushwa na uhujumu uchumi nchini.

**Mheshimiwa Spika;** Kwa upande mwengine ZAECA inaendeleza jitihada za mapambano dhidi ya rushwa na uhujumu uchumi ambapo imefanikiwa kufungua ofisi za Mikoa Unguja na Pemba. Kamati inaipongeza Mamlaka hii kwa uamuzi huo na inasisitiza kupitia ofisi za mikoa walizozianzisha kuwa na ofisi kamili, ikiwa ni pamoja na uwepo wa wafanyakazi wenye uwezo juu ya masuala ya uchunguzi wa masula ya uhujumu wa uchumi pamoja na kuwepo kwa vitendea kazi vya kutosha katika ofisi hizi.

**Mheshimiwa Spika;** kupitia taarifa za Udhibiti wa vitendo vya rushwa katika ukusanyaji wa mapato na matumizi ya Serikali, Kamati inasisitiza kulipa umuhimu sulala la malipo kwa njia ya kielektroniki ili kupunguza mianya ya rushwa nchini. Vile vile, kwa mwaka 2023, Kamati imeridhishwa na mpango wa Mamlaka wa kuimarisha mashirikiano na taasisi za Serikali na zisizo za kiserikali za ndani na nje ya nchi ili kuongeza ufanisi katika mapambano dhidi ya rushwa na uhujumu uchumi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri katika kufikia malengo haya Mamlaka iwashirishe viongozi wa ngazi zote wakiwemo masheha, Madiwani pamoja na Wawakilishi wa majimbo husika, kwa ajili ya kupata ufahamu wa sheria ndogo ndogo ambazo kukiukwa kwake ndio chanzo cha uhujumu uchumi katika nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika;** kwa kuongezea, Kamati inaipongeza kwa dhati kabisa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar kufanikiwa kuhamia katika jengo jipya liliyopo Kilimani Mnara wa Mbao mkabala na jengo la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF). Pamoja na kuwaombea kwa Serikali kuwapatia vitendea kazi vya kisasa ikiwemo vifaa vya uchunguzi ili waweze kurahisisha utendaji wa kazi zao.

**Mheshimiwa Spika;** kwa kumalizia, Kamati inaipongeza Mamlaka kwakuwa mstari wa mbele katika kuwasilisha Ripoti yao ya kila Mwaka kwa weledi na ufundi mkubwa kama sheria yao inavyooelekeza. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kufikiria kuendeleza juhudi zaidi katika mapambano dhidi ya rushwa na uhujumu uchumi kwa kuliingiza somo la Rushwa kwenye mitaala yetu kuanzia ngazi ya msingi ili chanzo na athari za rushwa ziweze kufahamika mapema katika jamii.

**Mheshimiwa Spika;** mwisho kabisa, naomba kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii ya maoni ya Kamati yetu ambapo ni wazi kuwa kila mmoja kmiongoni mwetu ameipata ripoti hii na kuisoma kwa umakini.

**Mheshimiwa Spika; Naomba Kuwasilisha.**

………………………………

(Mhe. Machano Othman Said)

Mwenyekiti,

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa

BARAZA LA WAWAKILISHI,

ZANZIBAR